**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA MAZISHI YA KISERIKALI YA HAYATI EDWARD NGOYAI LOWASSA, WAZIRI MKUU MSTAAFU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MONDULI, TAREHE 17 FEBRUARI, 2024**

- *Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;*
- *Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri wa Mkuu;*
- *Mheshimiwa Hemed Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais – Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*
- *Mhe. Dkt. Dotto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati;*
- *Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mhe. Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;*
- *Mama Regina Lowassa, Mjane wa Marehemu pamoja na Familia na Ndugu wote wa Marehemu;*

- *Mheshimiwa Fredrick Lowassa, Mbunge wa Monduli na mtoto wa Marehemu na Wabunge wa Mkoa wa Arusha na Wabunge wote mliopo nasi hapa;*
- *Waheshimiwa Viongozi Wakuu Wastaafu na Wenza wa Viongozi;*
- *Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;*
- *Makatibu Wakuu Viongozi, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;*
- *Waheshimiwa Mabalozi wanaowakilisha Nchi mbalimbali;*
- *Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;*
- *Mheshimiwa John Mongela, Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Wakuu wa Mikoa wengine mliopo;*
- *Ndugu Viongozi Mbalimbali wa Serikali*
- *Baba Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri na Viongozi wa Dini;*
- *Wazee wa kimila na Malaigwanaan*
- *Ndugu Wanahabari; na*
- *Waombolezaji wenzangu;*
- *Ndugu wananchi, Mabibi na Mabwana,*

*Tumsifu Yesu Kristo*
*Assalamu Aleykum*

***Utangulizi***

***Ndugu Wananchi*,**

Baada ya kutoa shukrani nyingi kwa Mwenyezi Mungu, niseme kwamba baadhi ya viongozi hubahatika kuandika vitabu vya mapito ya maisha yao ya kiuongozi, wangali hai. Wengine mapito yao huandikwa na watu wengine, ama wakiwa hai, au baada ya kutangulia mbele ya haki. Sisi Watanzania, tumepata bahati ya mapito na mchango wa viongozi wetu kuandikwa kwenye mioyo ya wananchi wote wa Tanzania. Hivi ndivyo historia ya ndugu yetu Edward Ngoyai Lowassa ilivyoandikwa pia.

Tumesikia salaam, risala na ushuhuda wa baadhi ya sura na kurasa za kitabu cha maisha ya ndugu yetu, Edward Lowassa kwenye mioyo na ndimi za Viongozi mbalimbali na wananchi kwa jumla. Nyuso za majonzi na mioyo ya simanzi ni taswira tosha ya aina ya maisha na historia aliyoiacha mpendwa wetu kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Pamoja na kwamba, msiba huu ni msiba wa Watanzania wote na maombolezo haya ni ya kitaifa, ila uhalisia ni kuwa, ukiwa, unyonge, majonzi na simanzi kubwa zaidi viko kwa familia, kwani imepoteza nguzo na mhimili muhimu katika maisha yao. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa pole kwa dada yangu, Mama Regina Lowassa, kwa watoto Fred, Pamela, Adda, Robert na Richard. Kwa kuwa alikwishajukuu, pia ninawapa pole wajukuu, familia na ndugu kwa ujumla. Msiba huu ni msiba wetu na simanzi zenu ni simanzi zetu. Hivyo tambueni hampo pekee yenu. Pigo hili ni pigo letu sote. Mkusanyiko wetu leo hii ni kuenzi mema yake na kusherehekea maisha yake.

Ninataka niungane na Baba Askofu (Gehaz) Malasusa, niwarudishe kwenye Kitabu cha Ayubu, Sura ya 14 Mstari wa 5, ambapo imeandikwa "kwa kuwa siku zake zimeamriwa, hesabu ya miezi yake unayo Wewe (yaani Bwana Mungu), Nawe umemwekea mipaka yake

asiyoweza kuipita". Nataka kuihusisha hii na msemo wa Kiswahili unaosema 'jitihada haizidi kudra'. Tumejitahidi sana kila pembe, lakini kudra ya Mungu imechukua nafasi yake. Mungu amemhitaji, amerudi kwa Muumba wake. Kama kitabu cha Ayubu kilivyosema, wote sisi siku zetu, hesabu zetu ziko kwa Mungu; hatuthubutu kupunguza wala kuongeza, na hakuna mwanadamu mwenye uwezo huo. Kwetu sisi ni kupokea na kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Kwa upande mwingine, Kama Taifa tumepoteza moja ya viongozi mahiri, mpenda maendeleo, mwanamageuzi na kipenzi cha wengi. Kipekee, natoa pole kwa wananchi wote kwa msiba huu mkubwa na mzito kwa Taifa letu. Kipekee, nitoe pole kwa wakazi wa Monduli na wa kijiji hiki (Ngarash) kwa kuondokewa na kiongozi, rafiki, ndugu na mmoja wenu ambaye pia kimila alikuwa ni Laigwaanan**.**

Vilevile nitoe pole kwa wananchi wote wa Tanzania kwa msiba huu mkubwa na mzito. Sote tuwe pole sana.

*Ndugu zangu,*

Shughuli yetu leo imekuwa nyepesi kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akisaidiwa na Mhe. Hemed Abdula, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na timu yao ya kitaifa. Wamefanya kubwa sana na nzuri sana. Nakushukuru sana Mhe. Waziri Mkuu na Wasaidizi wako kwa usimamizi mzuri.

Ninamshukuru pia Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye nilikuwa nimemuachia nchi.

Aidha, nawashukuru pia viongozi wa dini ambao mmekuwa pamoja na familia kwa maombi katika kipindi chote cha ugonjwa, hata alipotutoka mmeendelea kuomba, kuwafariji na kuwatia nguvu wafiwa.

Tunawashukuru jirani zetu na ndugu zetu wa Kenya wakiongozwa na Gavana (wa Kajiado Joseph Ole) Lenku

kwa kuja kutuunga mkono na kutupa nguvu katika msiba huu.

Kwa wanangu wasanii asanteni sana kwa nyimbo na tungo za kumuenzi mpendwa wetu. Wananchi na waombolezaji wenzangu asanteni kwa kujitokeza kwa wingi katika maeneo yote yaliyopangwa kuaga mwili na hata leo. Asanteni kwa sala na maombi yenu, hakika mmewatia nguvu na kuwapa faraja wafiwa.

***Maisha ya Lowassa kwa kifupi***

***Ndugu zangu,***

Kama tulivyokwishasikia katika wasifu wa Ndugu Edward Lowassa, alishika nyadhifa mbalimbali ndani ya Chama na Serikali hadi kufikia nafasi ya Waziri Mkuu. Aidha, **takribani nusu ya maisha yake yote ameyatumia katika utumishi na uongozi wa umma**. Alijitolea muda na maisha yake kwa ajili ya nchi yake, na kubeba dhamana ya

uongozi katika kila alikokabidhiwa. Aliweza kuacha alama kubwa na za kudumu katika kila jukumu lililomkabili.

Kupitia maisha yake, yapo mafunzo mengi kwetu sisi tuliobaki. Mengi yamekwishasemwa hapa na hata kabla ya leo, ikiwemo mapenzi makubwa kwa familia yake (nimemsikilia mwanagu Richard, ameonesha jinsi baba alivyokuwa na mapenzi kwa familia), imani yake kwa demokrasia na uhuru wa mawazo, na uchamungu wake. Mimi ningependa kugusia mafunzo matatu makubwa, ninayoona yana umuhimu mkubwa zaidi kwetu sote. Mambo hayo ni ushupavu, ustahilimivu, na ulezi.

***Ujasiri na ushupavu***

Ndugu yetu Edward Lowassa alikuwa kiongozi **jasiri na shupavu.** Aliuonesha ushupavu katika nyakati mbalimbali wakati wa uongozi wake. Alisimamia masuala yaliyokubalika ndani ya Serikali na yale aliyoagizwa na Chama bila kuyumba. Alipokuwa **Waziri wa Maji na**

**Maendeleo ya Uvuvi,** licha ya shinikizo kubwa kuhusu kutotumia maji ya Ziwa Victoria kwa sababu za kihistoria; **Kwa ujasiri na ushupavu mkubwa wa uongozi,** aliishauri vyema Serikali na kuweka msukumo, hadi sasa maji kutoka Ziwa Victoria yanatumika katika mikoa ya Shinyanga na Tabora. Leo hii, maji hayo sio tu yamefika katika mikoa hiyo, lakini tumeshaamua mradi huo ufike katika mikoa ya Singida na Dodoma.

Hayati Lowassa atakumbukwa pia kwa usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa uundwaji wa Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa zilizoleta mapinduzi makubwa katika utoaji wa huduma za maji safi na uondoaji wa majitaka.

Somo hapa ni kwamba, tukipewa dhamana za uongozi na kuaminiwa katika nafasi mbalimbali, ni lazima tuwe na uthubutu na ubunifu pamoja na kujitoa mhanga kusimamia na kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa weledi na uaminifu bila kukubali kuyumbishwa. Aidha, tunatakiwa kufanya kazi kwa bidii, kufuatilia utekelezaji

wa maelekezo ya viongozi wetu katika maeneo tuliyokasimiwa. Tusisubiri kusukumwa, na daima tuwe mbele ya wakati kuweza kuona mbali zaidi ya wale tunaowaongoza.

***Ulezi***

***Ndugu wananchi,***

Kwa waliomfahamu Edward Lowassa, na tumeona ushuhuda mbalimbali kupitia vyombo vya habari, watakubaliana nami kwamba alikuwa mlezi. Alikua Kiongozi mlezi aliyelea na kukuza wanasiasa vijana wengi ambao wanaendelea kulitumikia Taifa. Sifa hii ya ulezi na kuongoza vijana katika maisha yao ya kisiasa ilimjengea umaarufu na mapenzi miongoni mwa wengi. Kama alivyosema mdogo wangu, Freeman (Mbowe), yale matokeo ya kura ni kwa sababu hii, alijenga umaarufu mkubwa sana, yeye mwenyewe binafsi.

Katika kuweka msingi wa malezi, alipokuwa Mgombea Urais mwaka 2015 aliweka wazi kwamba, *kipaumbele chake cha kwanza kilikuwa elimu, cha pili elimu, na cha tatu elimu.* Maana yake alipenda vijana wapate maarifa na ujuzi kwa ajili ya ustawi wa familia zao na jamii kwa ujumla. Mheshimiwa Lowassa alikuwa **muumini wa elimu kama nyenzo ya kujikomboa na umasikini**, na mara zote alisisitiza kwamba, haupendi umasikini.

Nakumbuka aliwahi kusema '*Nimekuwa na nitaendelea kuwa mstari wa mbele katika kusisitiza umuhimu wa elimu bora na kwa wote, elimu inayowaandaa vijana kuingia kwenye soko la ajira la dunia'*.

Imani na msimamo wake katika elimu ndio ilimsukuma kusimamia kwa mafanikio Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) akiwa Waziri Mkuu katika Awamu ya Nne ya Uongozi wa Nchi hii. Mpango huu ulilenga kuongeza idadi ya wanafunzi

wanaopata elimu ya sekondari kwa kuratibu na kusimamia ujenzi wa shule za Sekondari katika kila Kata nchini. Licha ya maoni kinzani kutoka kwa baadhi ya wadau wa elimu, Lowassa **kama kiongozi anayejiamini na asiyeyumba katika kusimamia yale** yaliyokwishaamuliwa na Serikali, aliweza kusimamia kikamilifu kujenga shule za Sekondari za Kata.

Tangu wakati huo, Serikali imeendelea kusimamia ujenzi na uendelezaji wa shule za Kata kote nchini, na hivyo kuongeza shule za Serikali kutoka **828** mwaka 2004 hadi zaidi ya shule **5,000** mwaka 2023. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za Sekondari za Serikali imeongezeka kutoka wanafunzi **264,888** mwaka 2004 hadi kufikia wanafunzi **2,774,949** mwaka 2023.

Katika kufanyia kazi mawazo, maono yake, na kwa kutambua umuhimu wa elimu yetu kukidhi mahitaji ya soko la ajira, mwaka jana, Serikali imefanya maboresho ya Sera ya Elimu na Mitaala ya Elimu ili kuhakikisha elimu

inayotolewa inakidhi mahitaji ya sasa ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia.

Nikiuliza kwenye Umma huu waliopata malezi ya Lowassa, kuanzia hapa Monduli, Serikalini, Bungeni na Chamani - CCM mikono mingi sana itainuliwa. Alilea kwa kujenga na sio kwa kubomoa. Binafsi nilikutana nae serikalini nikiwa Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na nilikutana nae Bungeni nikiwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia nilikuwa naye kwenye Kamati Kuu ya CCM – nilijifunza mengi kwake. Kati ya hayo, nilichokiona kwa Mheshimiwa Lowassa ni, ukimheshimu, anakuheshimu.

***Ustahimilivu***

***Ndugu zangu,***

Nimezungumzia pia suala la ustahimilivu, ambalo ni jambo jingine la kujifunza kwa maisha ya ndugu yetu Edward Lowassa ni ustahimilivu. Katika mapito yake ya

kisiasa, aliwahi kuhama kutoka CCM kwenda CHADEMA ambako aliteuliwa kuwa mgombea Urais kwenye uchaguzi wa mwaka 2015.

Kama mlivyosikia, Lowassa alichipukia, kukulia na kulelewa CCM. Hata hivyo, alipofanya maamuzi ya kuhamia Chama kingine, aliendelea kunadi sera zake na kuifafanua dhana yake ya safari yake ya matumaini bila kumtukana, kumkejeli wala kumzushia mtu yeyote. Hata aliporudi CCM, hakuwahi kuwananga, kuwazodoa, kuwakebehi wala kuwasema vibaya wapinzani.

Hapa tunapata somo kubwa sana la siasa za kujenga hoja, kuheshimiana, kustahamiliana na siasa za kuleta maendeleo. Huo ni ukomavu mkubwa wa kisiasa na ni njia nzuri ya kuchukua kama tunataka kumuenzi Lowassa na vitendo vyake.

Alichotufundisha ni kwamba, tunaweza kutofautiana mitazamo, misimamo na sera, bila kutukanana, kurumbana wala kutikisa misingi ya utaifa na mshikamano wetu, na

bado tukaelewana. Sifa hii njema ndio iliyomfanya kujulikana kama mtu ambae aliweza kutunza urafiki wake na wengi.

Siku zote ni lazima Taifa tuliweke mbele zaidi ya itikadi za vyama vyetu. Ndio maana tulibuni falsafa ya R Nne, ambayo pamoja na mambo mengine, inatuelekeza kusimamia ustahimilivu na maridhiano. Tukistahimiliana na kuridhiana, Taifa letu litabaki salama na tutaendelea kulijenga kwa pamoja. Hivyo basi, tunao wajibu wa kuendelea kustahimiliana na kufanya siasa za kistaarabu, zinazoweka maslahi ya nchi mbele na zinazojadili masuala kwa hoja.

**Hitimisho**

***Ndugu zangu,***

Nikihitimisha, niseme kwamba yamesemwa mengi kuhusu mapito ya mpendwa wetu Ndugu Edward Ngoyai

Lowassa, tuendelee kumuenzi kwa kuyaishi yale mema aliyoyaamini na kuyasimamia.

Malipo ya watu wanaojitolea yamebainishwa kwenye msemo maarufu wa wasamaria wema usemao, ***'Duniani kuna watu wa aina mbili, watoaji na wapokeaji. Wapokeaji wanaweza kula vizuri, lakini watoaji hulala vizuri.'*** Lowassa alijitolea kwa nchi yake, kwa chama chake, kwa dini yake na kwa ndugu na rafiki zake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze yake mahala pema peponi, *Ameen!*

**BWANA alitoa, BWANA ametwaa; Jina la Bwana lihimidiwe!**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!**